# نَصَائِحُ فِيْ إِصْلَاحِ الْبُيُوْتِ

## حُقُوْقُ الزَّوْجِ عَلَى الزَّوْجَةِ

# NASAHA KATIKA KUTENGENEZA NYUMBA

## HAKI ZA MUME JUU YA MKE

**Mtunzi**

**Sheikh Khalid Dhahwi Ad-Dhafiiriy**

**(Allaah amhifadhi)**

**Tarjama**

**Abu Halima Arafaat Bin Mahmoud**

**(Allaah amsamehe yeye na wazazi wake)**

**بسم الله الرحمن الرحيم**

Naanza kwa jina la Allaah na Swala na Salamu Zimuendee Mtume wa Allaah, Jamaa zake, na kila mwenye kufuata mwongozo wake.

Ama baada ya yaliyotangulia: Allaah Subhanahu Wata'laa ametaja haki za mume na kadhalika Mtume wetu (Swala na Salamu Zimuendee), akalinyanyua jambo lake akabainisha kwamba haiwezi kuimarika nyumba yoyote isipokuwa kwa kusimama pande mbili hizi (mke na mume) kila mmoja akatimiza wajibu ilio juu yake kwa ajili ya Allaah na kutaraji ujira kutoka kwake, ili nyumba itulizane bila tabu yoyote na kudumu chini ya mwongozo wa Mtume (Swala na Salamu Zimuendee).

Allaah anasema:

﴿وَلَهُنَّ مِثْلُ ٱلَّذِى عَلَيْهِنَّ بِٱلْمَعْرُوفِ ۚ وَلِلرِّجَالِ عَلَيْهِنَّ دَرَجَةٌ﴾

**"Nao wanawake wanayo haki kisheria kama ile haki iliyo juu yao (kwa wanaume). Na wanaume wana daraja zaidi kuliko wao[1]".**

Allaah Subhaanah amebainisha kwamba wanaume wana haki juu ya wanawake na wana fadhila zaidi juu yao.
Na Mtume (Swala na Salamu Zimuendee) amebainisha haki za wanaume kwa ubainifu wa wazi kabisa, akasema:

«حَقُّ الزَّوْجِ عَلَى زَوْجَتِهِ أَنْ لَوْ كَانَتْ قَرْحَةٌ فَلَحَسَتْهَا مَا أَدَّتْ حَقَّهُ»

**"Haki za mume juu ya mke (ni kwamba) lau kungelikuwa na jeraha lenye usaha (mke) akaliramba bado hajatimiza haki zake[2]".**

[1]- Surat Al-Baqara/228.
[2]- Angalia kitabu: [Sahih Ibn Hibbaan (4164)].

Angalia namna gani Mtume (Swala na Salamu Zimuendee) amepiga mfano katika kutekeleza haki (za mume)!

Na pia amesema:

«لَوْ تَعْلَمُ الْمَرْأَةُ حَقَّ الزَّوْجِ مَا قَعَدَتْ مَا حَضَرَ غَدَاؤُهُ وَعَشَاؤُهُ حَتَّى يَفْرُغَ مِنْهُ»

**"Lau mwanamke angelijuwa haki za mume, basi asingekaa muda wa kumletea (kumtengea) chakula chake cha mchana na usiku mpaka amalize (kula[3]".**

Katika hadithi hii kuna ubainifu wa wazi juu ya haki anazostahiki mume kwa mkewe.

Na Mtume (Swala na Salamu Zimuendee) anasema:

«لَوْ أَمَرْتُ أَحَدًا أَنْ يَسْجُدَ لِأَحَدٍ، لَأَمَرْتُ الْمَرْأَةَ أَنْ تَسْجُدَ لِزَوْجِهَا»

**"Lau (ningeliweza) kumuarisha mtu yeyote kumsujudia mwingine, ningelimuamrisha mke kumsujudia mume wake[4]".**

Hadithi hii inabainisha ukamilifu wa utiifu, unyenyekevu, heshima na namna mke anavyotakiwa kutekeleza wajibu wake[5]. Na pia Mtume (Swala na Salamu Zimuendee) anasema kuhusiana na wanawake ambao wanawaudhi waume zao na wala hawatekelezi haki zao ipasavyo:

«لَا تُؤْذِي امْرَأَةٌ زَوْجَهَا فِي الدُّنْيَا، إِلَّا قَالَتْ زَوْجَتُهُ مِنَ الحُورِ العِينِ: لَا تُؤْذِيهِ، قَاتَلَكِ اللَّهُ، فَإِنَّمَا هُوَ عِنْدَكِ دَخِيلٌ يُوشِكُ أَنْ يُفَارِقَكِ إِلَيْنَا»

---

[3]- Angalia kitabu: [Al-Muujamul Kabiir (333)] na [Sahihili Jamii (9370)].

[4]- Angalia kitabu: [Sunan Ibn Maajah (1852)].

[5]- Amesema Ibn Battwaal: **"Kukufuru huduma zinazotolewa na mume ni kukufuru neema za Allaah, kwa sababu hizo zimetoka kwa Allaah zikapitia mikononi mwake".** Kitabu: [Kautharul maani Ddaraari (Jz. 2, Uk. 104)].

**"Hatomuudhi mwanamke yeyote (kumuudhi) mume wake duniani isipokuwa atasema mkewe miongoni mwa Huurul-ain (wanawake warembo wa peponi): Usimuudhi Allaah akulaani, kwa sababu yeye kwako wewe ni mgeni tu, anakurubia kukuacha na kuja kwetu[6]".**

Na hadithi za Mtume (Swala na Salamau Zimuendee) zimebainisha kwamba kumtii mume ni miongoni mwa sababu za kupata msamaha wa Allaah na kuingia peponi, kwa hiyo ni katika ibada iliyo bora. Imekuja katika hadithi ya Abu Huraira (Allaah amridhie):

« إِذَا صَلَّتِ الْمَرْأَةُ خَمْسَهَا، وَصَامَتْ شَهْرَهَا، وَحَفِظَتْ فَرْجَهَا، وَأَطَاعَتْ زَوْجَهَا قِيلَ لَهَا: ادْخُلِي الْجَنَّةَ مِنْ أَيِّ أَبْوَابِ الْجَنَّةِ شِئْتِ»

**"Pindi mwanamke atakaposwali swala zake tano, akafunga mwezi wake (ramadhani), akahifadhi tupu yake (na zinaa), na akamtii mume wake, ataambiwa: Ingia katika pepo kwa mlango wowote unaoutaka[7]".**

Kwa hiyo akitimiza mambo haya yaliyotajwa ataambiwa aingie peponi kwa mlango wowote anaoutaka, katika hili kuna ubainifu wa kuonesha fadhila za mambo haya na kwamba ni mambo yenye daraja kubwa mbele ya Allaah Subhaanah, na vilevile ni sababu ya kuingia peponi kupitia milango yake yote minane.

Na pia Mtume (Swala na Salamu Zimshukie) anasema:

«إِذَا دَعَا الرَّجُلُ امْرَأَتَهُ إِلَى فِرَاشِهِ فَأَبَتْ فَبَاتَ غَضْبَانَ عَلَيْهَا لَعَنَتْهَا المَلائِكَةُ حَتَّى تُصْبِحَ»

---

[6]- Angalia kitabu: [Sunan Tirmidh (1174)]. Anakusudia huyo ni sawa na mgeni aliyeshukia mahala kwa ajili ya kupumzika tu na baada ya muda ataendelea na safari yake kuelekea nyumbani kwake.

[7]- Angalia kitabu: [Sahih Ibn Hibbaan (4163)]. Ee Allaah, waongoze wake zetu katika usawa.

**“Pindi mwanaume atakapomuita mkewe kitandani kwake (kwa ajili ya jimai) akakataa, akalala (mume) hali ya kuwa amemkasirikia, basi Malaika wanamlaani mpaka apambaukiwe na asubuhi[8]”.**

Hilo ni kwa sababu ya kujiweka mbali na mume wake na kuacha kumtii, analala huku Malaika wa Allaah wanamlaani na Allaah anamchukia mpaka asubuhi.

Na Mtume (Swala na Salamu Zimshukie) alimuuliza mwanamke mmoja:

«أَذَاتُ زَوْجٍ أَنْتِ؟» قَالَتْ: نَعَمْ، قَالَ: «كَيْفَ أَنْتِ لَهُ؟» قَالَتْ: مَا آلُوهُ إِلَّا مَا عَجَزْتُ عَنْهُ، قَالَ: «فَانْظُرِي أَيْنَ أَنْتِ مِنْهُ، فَإِنَّمَا هُوَ جَنَّتُكِ وَنَارُكِ»

**“Je wewe una mume?” akasema: ndio, akamuuliza: “vipi wewe (katika kumtimizia) yeye haki zake?”, akasema: sifanyi mapungufu ila kwa lile nisiloliweza, akasema: “basi zingatia iko wapi nafasi yako kuhusu yeye kwa sababu yeye ndio pepo yako na moto wako[9]”.**

Maana yake ni kwamba (utaingia peponi) kutokana na nafasi yako kwake katika kumtii yeye, lakini hapa inakusudiwa kumtii katika yasiyokuwa mambo ya kumuasi Allaah.

Na Mtume (Swala na Salamu Zimmuendee) amesema kuhusiana na mwanamke mwenye kumuasi mume wake:

«اثْنَانِ لَا تُجَاوِزُ صَلَاتُهُمَا رُءُوسَهُمَا: عَبْدٌ أَبَقَ مِنْ مَوَالِيهِ حَتَّى يَرْجِعَ إِلَيْهِمْ، وَامْرَأَةٌ عَصَتْ زَوْجَهَا حَتَّى تَرْجِعَ»

---

[8]- Angalia kitabu: [Sahihil Bukhari (3237) na Muslim (1436)].
[9]- Angalia kitabu: [Al-Musnad (19003)].

**"Watu wa aina mbili hazivuki swala zao (juu ya) vichwa vyao, mtumwa ambaye amewakimbia mabwana zake mpaka atakaporejea, na mwanamke ambaye amemuasi mume wake mpaka akirejea (kumtii mume wake)[10]".**

Anaswali lakini Allaah hakubali swala yake wala hapati ujira.

Na pia amebainisha kwamba Allaah hamuangalii kwa jicho la huruma mwanamke ambaye hamsifu wala kumshukuru mume wake kwa huduma na mahitaji mbalimbali anayomfanyia.

«لا يَنْظُرُ اللهُ إِلَى امْرَأَةٍ لا تَشْكُرُ لِزَوْجِهَا وَهِيَ لا تَسْتَغْنِي عَنهُ»

**"Allaah hamuangalii (kwa huruma) mwanamke ambaye hamshukuru mume wake, na hali ya kuwa hajitoshelezi kumuacha yeye[11]".**

Kwa ajili hiyo Mtume (Swala na Salamu Zimuendee) amemsema vibaya wanawake wenye sifa hizi, kukufuru huduma anazopatiwa na mume wake, (mke) utamtendea wema na hisani kwa muda mrefu, lakini akipata kutoka kwako jambo ambalo halimpendezi au kero yoyote atasema: (sijaona kutoka kwako wema wowote), ndiyo maana Mtume (Swala na Salamu Zimuendee) akaweka wazi kwamba hii ni tabia mbaya na pia ni sababu ya mwanamke huyo ambaye hamshukuru mume wake kukosa rehma za Allaah.

Amesema Sheikhul islaam Ibn Taymiyyah (Allaah amrehemu):

(وَلَيْسَ عَلَى الْمَرْأَةِ بَعْدَ حَقِّ اللَّهِ وَرَسُولِهِ أَوْجَبَ مِنْ حَقِّ الزَّوْجِ )

---

10- Angalia kitabu: [Silsila Ahaadithi Ssahiha (288)].
11- Angalia kitabu: [Silsila Ahaadithi Ssahiha (289)].

**“Hakuna juu ya mwanamke baada ya (kutekeleza) haki ya Allaah (jambo la) wajibu zaidi kuliko (kutekeleza) haki ya mume[12]”.**

Kwa hiyo ni wajibu juu ya wanawake kuzingatia haki hizi na kufahamu kwamba kumtii mume ni sababu ya kuridhiwa na Allaah Subhaanah na kupata malipo makubwa kutoka kwake, mpaka uwe ni mwanamke mwema, bora, mwenye kupigiwa mfano na kuigwa kwa wema wake, muamala, na malezi ya familia.

Anasema Imam Ahmad (Allaah amrehemu):

(أَقَامَتْ مَعِيْ أُمُّ صَالِحٍ ثَلَاثِيْنَ سَنَةً فَمَا اخْتَلَفْتُ أَنَا وَهِيَ فِيْ كَلِمَةٍ)

**“Nimeishi pamoja na Ummu Swaaleh miaka thelathini sijawahi kutafutiana nae kwa neno lolote[13]”[14].**

Huu ni mfano wa mwanamke mwema ambaye anamtii mume wake, kwa sababu wema wa mwanamke haupo kwenye mali, cheo wala nasaba/ukoo, bali ni kama alivyosema Mtume (Swala na Salamu Zimuendee):

«خَيْرُ النِّسَاءِ الَّتِي إِذَا نَظَرْتَ إِلَيْهَا سَرَّتْكَ، وَإِذَا أَمَرْتَهَا أَطَاعَتْكَ، وَإِذَا غِبْتَ عَنْهَا حَفِظَتْكَ فِي نَفْسِهَا وَمَالِهَا»

**“Mwanamke bora yule ambaye ukimtazama anakufurahisha, ukimuamrisha anakutii, na unapokuwa mbali naye anakuhifadhi katika nafsi na mali yako[15]”.**

---

[12]- Angalia kitabu: [Majmuul Fataawa (Jz. 32, Uk. 275)].
[13]- Angalia kitabu: [Taareikh Baghdad (Jz. 14, Uk. 438)].
[14]- Huyo ni mkewe A’bbaasa Bint Fadhli ambaye alizaa naye mtoto mmoja tu (Saaleh).
[15]- Angalia kitabu: [Musnad At-twayaaalis (2444)].

Huyu ndiye mwanamke mwema, anajichunga na maovu, anawatunza watoto wake, anatunza mali ya mume wake, hafanyi ubadhirifu katika matumizi na kufuja mali, na pia anapokuwa mbali naye anajichunga, anasimamia nyumba wala hautasikia ndani ya nyumba hiyo isipokuwa kheri tupu.

Isitoshe Mtume (Swala na Salamu Zimuendee) amefikia kubainisha kwamba hata ibada za sunnah mwanamke hawezi kuzitekeleza isipokuwa kwa idhini ya mume wake:

«لاَ يَحِلُّ لِلْمَرْأَةِ أَنْ تَصُومَ وَزَوْجُهَا شَاهِدٌ إِلَّا بِإِذْنِهِ، وَلاَ تَأْذَنَ فِي بَيْتِهِ إِلَّا بِإِذْنِهِ، وَمَا أَنْفَقَتْ مِنْ نَفَقَةٍ عَنْ غَيْرِ أَمْرِهِ فَإِنَّهُ يُؤَدَّى إِلَيْهِ شَطْرُهُ»

**"Si halali kwa mwanamke kufunga (saumu) na hali ya kuwa mume wake yupo (katika mji) isipokuwa kwa idhini yake, wala asimruhusu kuingia nyumbani kwake (mtu ambaye mume wake hamridhii) isipokuwa kwa idhini yake[16], na mali yoyote aliyoitoa sadaka bila ya idhini ya mume wake basi atapewa yeye (mume) nusu yake[17]"[18].**

---

16- Haifai kwa mwanamke kumuingiza ndani ya nyumba yake mtu ambaye anafahamu kwamba mume wake haridhii mtu huyo kuingia nyumbani kwake hata kama ni ndugu wa karibu awe ni mwanaume au mwanamke, lakini wanawake wengi hili hawatekelezi matokeo yake atamruhusu mtu kuingia ndani kwa sababu anajua mume wake hatorudi nyumbani kwa muda huo!.

17- Angalia kitabu: [Sahihil Bukhari (5195)].

18- Ikiwa mwanamke amepewa ruhusa na mume wake kutoa sadaka ima chakula au pesa basi ni vizuri mwanamke huyo akajichunga katika utoaji wake wala asipitilize kiwango cha kawaida (Ada), akamaliza mpaka pesa ya matumizi ya wajibu nyumbani kwake, hakika kufanya hivyo ni makosa na akitoa kiasi kile cha kawaida atapata ujira yeye (kwa kutoa kwake) na mumewe ambaye ndiye mmiliki wa asili ya mali iliyotolewa. Na pia kuna ruhusa ya jumla kama kusema: **"Msaidie mtu yeyote mwenye shida"** au ruhusa ya kudhibitiwa: **"Usitoe zaidi ya shilingi (2000) au kilo 2 n.k"**, kwa hiyo usizidishe zaidi ya kiwango hicho isipokuwa kwa idhini yake, na akitoa chochote katika mali ya mume wake bila idhini yake atapata madhambi. **Zingatieni hili.**

Kwa ajili hiyo amesema Ibnul Jauziy (Allaah amrehemu) hali ya kuwapa nasaha wanawake:

(وَيَنْبَغِيْ لِلْمَرْأَةِ العَاقِلَةِ إِذَا وَجَدَتْ زَوْجاً صَالِحاً يُلَائِمُهَا أَنْ تَجْتَهِدَ فِيْ مَرْضَاتِهِ، وَتَجْتَنِبَ كُلَّ مَا يُؤْذِيْهِ، فَإِنَّهَا مَتَى آذَتْهُ، أَوْ تَعَرَّضَتْ لِمَا يَكْرَهُهُ أَوْجَبَ ذَلِكَ مَلَالَتَهُ، وَبَقِيَ ذَلِكَ فِيْ نَفْسِهِ، فَرُبَّمَا وَجَدَ فُرْصَتَهُ فَتَرَكَهَا أَوْ آثَرَ غَيْرَهَا، فَإِنَّهُ قَدْ يَجِدُ، وَقَدْ لَا تَجِدُ هِيَ، وَمَعْلُوْمٌ أَنَّ المَلَلَ لِلْمُسْتَحْسِنِ قَدْ يَقَعُ، فَكَيْفَ لِلْمَكْرُوْهِ؟).

**"Inapasa kwa mwanamke mwenye akili akipata mume mwema anaemfaa ajitahidi kumridhisha (kumfurahisha) na kujiepusha na kila lenye kumchukiza, kwa sababu yeye wakati wowote atakapomuudhi au kufanya jambo lenye kumchukiza litapelekea hilo kumhuzunisha/kuchoka na litabaki hilo ndani ya moyo wake, na huenda huyo (mume) akapata fursa yake akamuacha au akamfadhilisha mwingine, kwa sababu huenda huyo (mume) akampata (mke mwingine) na yeye (mke) huenda asipate (mume kama huyo), na ni jambo lenye kujulikana kwamba kuchoshwa huenda kukapatikana hata kwa mwenye kutenda wema basi vipi kwa mwenye kuchukiza?![19]".**

Na mwanaume vilevile akimpata mke mwema basi amuweke katika himaya yake na atoe bidii katika kutengeneza nyumba yake, na kadhalika mwanamke akipata mume mwema alazimiane naye, na kumridhisha katika mambo ambayo Allaah amewajibisha kwake (kumtendea mume wake) kwa ajili ya kutafuta radhi za Allaah.

---

[19]- Angalia kitabu: [Ahkaamu Nnisaa (Uk. 145)].

Allaah anasema:

﴿فَٱلصَّٰلِحَٰتُ قَٰنِتَٰتٌ حَٰفِظَٰتٌ لِّلۡغَيۡبِ بِمَا حَفِظَ ٱللَّهُۚ﴾

**[Basi wanawake wema ni wale wenye kutii, wanao jilinda hata katika siri (wakiwa mbali na waume zao) kwa vile Allaah alivyoamrisha wajilinde[20]].**

Allaah amewasifia wanawake wenye kuwatii waume zao na wenye kuhifadhi siri za waume zao, kwa maana hawatangazi siri ambazo wamepewa na waume zao au hawawataji wao kwa ubaya pindi wanapokuwa hawapo na wala hawaenezi yale mambo ya siri yenye kutendeka baina yao.

Na Mtume (Swala na Salamu Zimshukie) amebainisha adhabu ya mwanamke mwenye kumuomba talaka mumewe na kutaka kutengana naye bila ya ubaya wowote aliomfanyia:

«أَيُّمَا امْرَأَةٍ سَأَلَتْ زَوْجَهَا طَلَاقًا فِي غَيْرِ مَا بَأْسٍ، فَحَرَامٌ عَلَيْهَا رَائِحَةُ الْجَنَّةِ»

**"Mwanamke yeyote atakaye muomba mume wake talaka bila ya ubaya wowote (aliomtendea) basi ni haramu juu yake harufu ya pepo[21]".**

Hii ndio adhabu ya mwanamke ambaye ameomba talaka ili kuachana na mume wake bila sababu za kisheria (sababu za msingi), siku ya kiama hapati harufu ya pepo. Pia afahamu mume kwamba yeye ndiye msimamizi na ni mwenye kuulizwa kuhusiana na mke na watoto, kadhalika mke afahamu kwamba ameamrishwa kumtii mume wake na kuilea vizuri familia yake na kutoa juhudi katika kutengeneza nyumba yake.

---

[20]- Surat An-Nisaa/34.

[21]- Angalia kitabu: [Sunan Abi Daud (2226)].

Mtume (Swala na Salamu Zimshukie) amesema:

«كُلُّكُمْ رَاعٍ، وَكُلُّكُمْ مَسْئُولٌ عَنْ رَعِيَّتِهِ، ... وَالرَّجُلُ رَاعٍ فِي أَهْلِهِ وَهُوَ مَسْئُولٌ عَنْ رَعِيَّتِهِ، وَالمَرْأَةُ رَاعِيَةٌ فِي بَيْتِ زَوْجِهَا وَمَسْئُولَةٌ عَنْ رَعِيَّتِهَا...»

**"Nyote ni wachunga (wasimamizi) na kila mmoja ataulizwa kuhusu alichokichunga, … mwanaume ni mchunga kwa ahli zake (mke, watoto n.k) na ataulizwa kuhusu alichokichunga, na mwanamke ni mchunga katika nyumba ya mume wake na ataulizwa kuhusu alichokichunga[22]".**

Allaah ndiye mjuzi zaidi[23].

Namuomba Allaah A'zza Wajalla awajaalie wake na watoto wetu kuwa wema na atusamehe sisi pamoja na wazazi wetu.

Swala na Salamu Zimshukie Mtume wetu Muhammad.

**Markaz Sheikhil islaam Ibn Taymiyyah**

**7/rajab/1441H - 31/3/2020M.**

**Pongwe/Tanga**

**Tanzania.**

**Simu: 0715263253.**

[22]- Angalia kitabu: [Sahihil Bukhari (893)].

[23]- Sheikh Ad-Dhafiir (Allaah amhifadhi) amezitaja hadithi na maneno mbalimbali ya Maulamaa kuhusiana na maudhui hii bila kuashiria sehemu zake, nikaona nitaje Kitabu, Juzuu na Ukurasa ambayo hupatikana maneno hayo kwa faida na kumfanyia wepesi yule anaetaka ziada.